JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA SEKONDARI DAREDA
S.L.P 344, BABATI-MANYARA

School e-mail daredaschool81@gmail.com

Simu: ***Mkuu wa Shule*** 0785133121/0754045985 au

Makamu mkuu wa shule au 0758946290

Matron 0784376499

Kumb.Na.DRD/SS/DED/BBT/JIF/F.5/Vol.1

MZAZI/MLEZI WA: .....

S.L.P .....

.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI DAREDA WILAYA YA BABATI MKOA WA MANYARA MWAKA 2022.

1:0 UTANGULIZI:

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kuendelea na masomo ya Sekondari Kidato cha Tano (v) mwaka 2022/2023 Tahasusi ya.....Shule ina Tahasusi (3) ambayo ni HGL/HKL na CBG.

Shule itafunguliwa tarehe ***rasmi iliyotangazwa na Serikali*** ili kuanza masomo mara moja kwa mwaka wa masomo 2022/2023.

Mzazi/mlezi hakikisha ***unamleta mwanao mwenyewe*** ili aweze kuandikishwa tarehe iliyotajwa bila kukosa***,mwanafunzi bila mzazi hapokelewi***

Ni muhimu sana mzazi/mlezi kumfikisha mwanao hadi hapa shuleni.

N.B Siku na saa ya mwisho ya kuripoti ni tarehe rasmi ya Serikali kuanzia asubuhi hadi saa. 10.00 Jioni .

HONGERA SANA! ! !

Shule ya Sekondari Dareda ipo katika Kijiji cha Loto Kata ya Dareda,Tarafa ya Bashnet,Wilaya ya Babati Vijijini katika Mkoa wa Manyara.Umbali wa kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara(Babati) hadi Shule ni Km 32 kufuata barabara iendayo singida.Shule ipo karibu sana na Hospitali kubwa ya Dareda inayomilikiwa na Jimbo Katoliki la Mbulu.Kwa Wanafunzi wanaotokea Arusha,Tanga,Dar-es Salaam na mikoa jirani ukifika Babati Mjini tafuta mabasi yaendayo Dareda Mission kupitia Dareda Centre na ukishuka Dareda Mission uliza Shule ya Dareda Sekondari iko umbali wa mita 700 kutoka Stendi ndogo ya Mabasi upande wa Kusini Magharibi.Kwa wale watokao kanda ya ziwa kanda ya Magharibi,kanda ya nyanda za juu na kanda ya kati panda mabasi yaendayo Arusha kupitia Singida na ushuke Dareda Centre ambapo utapata magari yaendayo Dareda Mission au mbulu.Kutoka Centre kuna umbali wa kilomita nane (8) na ukifika Dareda Mission shuka na uliza shule ya Sekondari Dareda ilipo.Ufikapo shuleni nenda katika ofisi ya Mkuu wa shule ili upokelewe na utapewa maelezo mengine.

Nawatakia safari njema!!!!!

KARIBU SANA.

2:0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**.

2:1 ***ADA NA MICHANGO MINGINE***.

- Ada ya shule ni Tshs **70,000/=** kwa mwaka (**Tshs 35,000/=)** kwa muhula)
- Mchango wa Maendeleo ya Taaluma Tshs.(20,000/=) kwa muhula (40,000/=) kwa mwaka.
- Mchango wa ukarabati wa Samani Tshs 20,000/=hulipwa mara moja tu.
- Tshs 5,000/=kwa ajili ya tahadhari hulipwa mara moja tu(***haitarejeshwa***)
- Tshs 6,000/=kwa ajili ya kitambulisho cha Shule hulipwa mara moja tu.
- Mchango wa maji safi na salama Tshs 5000/= kwa mwaka
- Mchango wa Ulinzi,Wahudumu wa Ofisi,Wapishi (20,000/=) kwa muhula (40,000/=) kwa mwaka.
- Nembo ya Shule Tshs.2,500/= mara moja.
- Rim paper nne (04) karatasi size A4 (Duplicating paper) 2 kwa muhula 4 kwa mwaka.

  Jumla ni Tshs. **113,500/=** kwa muhula wa kwanza kwa muhula wa pili Tshs**.75,000/=** Jumla ya fedha zote ambazo zinatakiwa kulipwa kwa mwaka 2022/2023 ni shilingi laki mbili na elfu tano na mia tano tu kwa mwaka.

  Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya Shule na. **40701200091 NMB** tawi la Babati jina la Akaunti ni Dareda Secondary School Fund.

  Utatakiwa kuleta Bank pay in slip (BPS) iliyoandikwa jina kamili la Mwanafunzi na sio jina la Mzazi/Mlezi au aliyetuma fedha.

  Angalizo: Hatupokei fedha taslim na fedha zikishawekwa kwenye Akaunti ya Shule hazirejeshwi.

3:0 ***SARE ZA SHULE***.(Mzazi utawajibika kumshonea Mwanao Sare zote za Shule zinazotakiwa)

3:1**. WAVULANA**.

a) Suruali mbili (kitambaa kimeambatanishwa) ***Rangi ya kitambaa Sky Blue*** zenye mfuko wa nyuma mmoja wenye kuingia ndani,looks 8 yaani mbele nne (kushoto mbili na kulia mbili),nyuma mbili na pembeni mbili.Vile vile iwe na marinda manne (4 Celebrations) mbili kila upande na tai mbili kwa ajili ya Sare za Shule sawa na Rangi ya Kitambaa cha Suruali.Suruali za mlegezo,zinazobana (Chupa) haziruhusiwi Shuleni.
b) Unatakiwa kuwa na masharti mawili meupe mikono mirefu aina ya tetroni (siyo Cotton) zinazofaa kufunga Tai yenye Mifuko.
c) Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
d) Mkanda wa Suruali ambao ni Nyeusi.
e) Shuka mbili rangi moja ya Blue Bahari.

3:2 WASICHANA.

a) Sketi mbili ziwe ndefu hadi chini ya fundo za miguu zenye marinda ishirini belti(pindo dogo la kiuno) nchi mbili Kitambaa cha Sketi kimeambatishwa.***Rangi ya kitambaa Sky Blue***
b) Blauzi mbili nyeupe za mikono mirefu aina ya tetroni zinazofaa kufunga tai na ziwe na mfuko mmoja tu.Cotton haitakiwi.
c) Soksi jozi mbili stocking za rangi nyeupe.
d) Shuka mbili rangi moja ya pink.
e) Pea moja ya khanga au kitenge.
f) Iwapo mwanao ni mwislamu sare ya shule itakuwa ni:-
- ″Short″ Kanzu mbili (2) nyeupe urefu ni inchi kumi na mbili (12) kutoka nchini na isiwe na mipasuo pembeni.

- Hijabu mbili (2) ″Vitambaa vya kufunika Kichwa na Mabega nyeupe visivyo na Marembo yeyote″

3:3 **NGUO NA VIFAA VYA JUMLA**.

a) Sweta mbili(***Rangi ya Sweta sawa na kitambaa cha sketi na suruali***) ***Sky Blue***
b) Track Suit jozi mbili zenye Rangi nyeusi na michirizi nyeupe inayoshuka kutoka Begani hadi chini.
c) Kibanio kimoja cha Tai.
d) Godoro size 2½ x3x6, Blanketi moja,Mto/Foronya 2 zenye Rangi inayofanana na shuka.
e) Chandarua nyeupe
f) Pasi ya Mkaa kwa ajili ya kunyoosha Nguo.
g) Taa ya sola ya kuchaji na jua kwa ajili ya kutumia wakati Umeme unapokatika.
h) Taulo moja, sabuni za kuogea za kutosha malapa
i) Sabuni ya Unga ya kutosha kwa ajili ya kufulia.
j) Sanduku moja imara la Bati lenye kufuli
k) Kila mmoja aje na barakoa 2 za Kitambaa cha Pamba (Cotton)
l) Viatu jozi mbili Rangi nyeusi vya Ngozi na vyenye kufunga kwa Kamba (Gidamu) visivyo na Kisigino kirefu.Viatu vinavyojulikana kama Bajaji haviruhusiwi.

3:4 **NGUO ZA MICHEZO**.

i) Wavulana.
   (a) Raba Jozi moja Njumu Nyeusi
   (b) Bukta moja na T-Shirt moja ya light blue isiyo na ushabiki wa timu yoyote (yaani isiyo na maandishi)
ii) Wasichana.
   a) Raba jozi moja nyeusi
   b) Bukta moja na T-shirt moja isiyo na ushabiki wa timu yoyote (yaani isiyo na Maandishi

NB: Mwanafunzi aje na sare ya shule alikotoka akifika atashonea sare maeneo ya shule

ANGALIZO.Uvaaji wa Sare ya Shule ni muhimu na ni lazima uwe na Sare ya Shule yenye heshima na utakaguliwa ukifika Shuleni kama tunavyokuagiza katika Fomu hii.Sare ya Shule itatumika wakati wa masomo,ukiwa nje ya Shule kwa ruhusa na Safarini kuja Shuleni na kurudi Nyumbani wakati wa Likizo.

3:**5 MAAGIZO MENGINE**.

1. Madaftari Makubwa (Counter Books Quire Four) yasiyopungua kumi.
2. Kalamu,rula,Mkebe na Vifaa vya mahesabu Mathematical Set),Scientific Calculators Non Programmable with the function ranging from fx82 to fx 991 MS and Mathematical Table with no formulae na ***seti ya Disecting kit" kwa Wanafunzi wa CBG.***
3. Ndoo mbili ya plastic yenye ujazo wa lita 10-wote.
4. Jembe moja jipya lenye mpini.
5. Vitabu binafsi vya masomo kulingana na tahasusi (Combination) yako.
6. T-Shirt yenye Nembo ya Shule Tshs **12,000/=** kwa kila Mwanafunzi.
7. Kila Mzazi ahakikishe amempatia mwanao Kitambulisha cha Bima ya Afya kwa ajili ya Matibabu ili kuepuka usumbufu, ikiwezekana amkatie Bima ya Afya ya mwaka mmoja(Kitambulisho cha Bima ya Afya kwa watoto watumishi ni bora zaidi).

8. Kutokana na shule kutokuwa na gari tunashauri kila mzazi achangie **10,000/=** kwa temu .
9. Tshs **10,000/=** kwa ajili ya Mahafali.

3:**6 MAVAZI YA KAZI**.

- Sketi mbili (2) nyeusi nzito Mshono kama Sketi za Darasani
- Suruali mbili (2) nyeusi mshono kama Suruali za Darasani.
- Raba nyeusi (Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala nje ya Bweni au Darasani ama jikoni)

NB: Ndala zitatumika ndani ya Bweni tu kwa matumizi ya kuoga.

Vazi la kazi litavaliwa na ″T-shirt″ yenye nembo ya shule ambayo inapatikana shuleni.

3:7. Mavazi kwa ajili ya kuzuia baridi (nje ya Darasa)

- Pull Neck mbili(2) zisizo na maandishi wala madoido yoyote.

3:8 **VIFAA VYA USAFI**

CBG :Aje na Panga jipya lililonolewa,jembe jipya lenye mpini imara,Squeezer

1 pamoja na Ufagio aina ya chelewa.

HGL: Aje na ″Soft Broom″ Jembe jipya lenye mpini imara,Squeezer 1 pamoja na Ufagio aina ya chelewa

HKL: Aje na Kwanja jipya lililonolewa,Jembe jipya lenye mpini imara,Hard Broom pamoja na Ufagio aina ya chelewa.

NB:1 Kila Mwanafunzi aje na **Tshs.5000/=** kwa ajili ya kununulia Madawa ya Chooni wakati wa Usafi.

2. Kutokana na kikao cha wazazi tarehe **28.01.2022**,wameazimia kuwamotisha walimu kwa tshs 30,000 kwa term baada ya kuridhishwa na juhudi zao na matokeo ya Taifa kidato cha sita 2020.

ANGALIZO: Taa ya Sola inayotumia mwanga wa jua itasaidia iwapo Umeme utakatika wakati Mwanafunzi akiwa Darasani au Bwenini nyakati za usiku.

3:**9 VIFAA VYA BWENINI**.

- Godoro moja (1) inchi 2½ ×3×6 .(hakikisha iwe original)
- Aje na shuka mbili (2) rangi ya Blue Bahari kwa Wavulana na shuka mbili (2) Pinki kwa Wasichana.
- Aje na mto mmoja (1) pamoja na Foronya mbili (02) zenye rangi kulingana na shuka lake.
- Aje na Blanketi moja (1) zito.
- Aje na Taulo moja (1)
- Aje na Sanduku la Chuma moja (1) (Tranka) lenye kufuli imara.
- Aje na chandarua Rangi nyeupe au Blue, umbo la pembe nne kwa ajili ya kujikinga na Mbu.
- Aje na Doti moja ya Kitenge kwa Wasichana kwa ajili ya kuongea tu pamoja na Ndala.

- Aje na dawa ya Meno, Mswaki na Mafuta ya kujipaka.(Haruhusiwi kutumia Vipodozi vya aina yoyote ile na mapambo.

4:0 VYOMBO VYA CHAKULA.

- Aje na Sahani ya Bati (″Alluminium) moja (1)
- Aje na Bakuli moja (1) bati.
- Aje na Kikombe kimoja (1) Bati.
- Aje na Kijiko kimoja (1)

***NB*: Vyombo vya plastic haviruhusiwi kabisa.**

4:1 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI.

Mzazi /Mlezi unaweza kumpatia Mwanao kiasi kidogo cha fedha kulingana na mahitaji yake madogo madogo ya lazima.Haruhusiwi kuja na fedha nyingi na iwapo kuna ulazima wa kumtumia Mwanao fedha kwa matumizi yake binafsi tumia njia ya Simu ya Mkuu wa Shule,M-pesa/Airtel Money.

Angalizo:-Mzazi/Mlezi huruhusiwi kabisa kutumia Akaunti ya Shule, Mabasi kutuma fedha kwa ajili ya matumizi binafsi ya Mwanao

4:2 MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI.

- Wakati wa usajili Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo kwa ajili ya uthibitisho:-
  - Sare ya Shule (Full School Uniform)
  - Barua yake ya maagizo (Joining Instruction)
  - Vyeti vyake halisi (originals) na vivuli (Photocopies) ya vyeti vya Taaluma Kidato cha nne (IV) pamoja na Leaving Certificate (Cheti cha kuhitimu Kidato cha nne (IV)
  - Vitabu kulingana na tahasusi aliyopangiwa.
  - Cheti cha kuzaliwa halisi na Kivuli chake
  - Barua ya Mzazi/Mlezi ya kukubali nafasi hii ikiwa imejazwa kikamilifu. (Kiambatisho B)
  - Cheti cha Daktari (Medical Examination Form) ambacho kimejazwa vizuri na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali na siyo Hospitali binafsi. (Kiambatisho C)

ANGALIZO:

- Nyaraka zilizotajwa hapo juu ni muhimu sana tafadhali njoo nazo bila kukosa.
- Utasajiliwa Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule.
- Utawasilisha nyaraka zote za fedha Ofisi ya Mhasibu.
- Utawasilisha Vifaa vyote kama:-Jembe,Ndoo, Squeezer,Hard Broom,Rim pamoja na Vifaa vingine katika Ofisi ya Afisa Manunuzi

ONYO!!!

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na Nguo za Nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda Bwenini kabla ya kukamilisha Usajili wake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na Simu ya Mkononi au Kitu chochote kinachohusiana na Simu,iwapo atakamatwa na Simu au Kifaa chochote cha simu atanyang'anywa na **KUFUKUZWA SHULE** (hatarejeshewa simu au vifaa hivyo)
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote ile Shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vitu kama pasi,heater,kibatari,karabai,mishumaa,radio,camera,television,jiko lolote la kupikia na Sufuria,Chupa za Chai.***NI MARUFUKU***.

- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa shule kwa tarehe iliyopangwa na iwapo atachelewa kwa muda wa siku saba (7) baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti bila taarifa ya maandishi atakuwa amepoteza nafasi yake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndefu,kucha,Kope za bandia,kupaka rangi kwenye kucha,Lipstick,Wanja,kuweka Dawa kwenye Nywele,kutumia Vipodozi na haruhusiwi,kusuka Nywele, hivyo atatakiwa kunyoa Nywele zake na ziwe fupi muda wote kwa Wastani wa kuchana kwa kutumia Kitana kidogo.
- Mwanafunzi anatakiwa:-kusoma,kuelewa kuzishika na kuzifuata Sheria za Shule ambazo atafafanuliwa mara tu afikapo Shuleni.Baadhi ya Sheria hizo zimeambatishwa pamoja na Form hii.
- Ni vyema Mwanafunzi asindikizwe na Mzazi/Mlezi wake ili Mzazi au Mlezi huyo afahamu Mazingira ya Shule na Mahali Shule ilipo na vilevile kufahamiana na Watumishi wa Shule na kuwa na uhakika ya kuwa Mtoto wake amefika Salama mahali panapostahili.
- Aidha Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake Na 10 mwaka 1995 vilevile Shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Kwa kifupi Mwanafuzi azingatie mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kina mara tu afikapo Shuleni:-

(i) Mwanafunzi atatakiwa:

- Kuheshimu Viongozi,Wazazi, Wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla.
- Kuhudhuria vizuri shughuli zote za ndani na nje ya Darasa au ya Shule
- Kutekeleza kwa makini na kwa uaminifu na uadilifu mkubwa shughuli zote za Shule kama ilivyo kwenye Ratiba.
- Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine atakazo pangiwa
- Kukimbia mara aitwapo na mtu anayemzidi umri.
- Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelezo yote juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Uanafunzi wake katika Shule hii.
- Kutunza Usafi wa Mwili na Mavazi pamoja na mazingira yote ya Shule.
- Kuvaa Sare ya Shule iliyo Ndefu na Safi wakati wote anapokuwa ndani au nje ya mipaka ya Shule.
- Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote ambapo Ratiba ya Shule huanza saa **11:00 alfajiri kwa mchakamchaka na kuishia saa 4:30 usiku baada ya Ukaguzi (Bed Checking) ambapo taa zote za ndani ya Mabweni na Madarasa huzimwa na Wanafunzi kulala.**

(ii) MAMBO/MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi wa aina yoyote
2. Uasherati,Ushoga na Usagaji
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile Bangi, Mirungi, Cocaine,Mihadarati na Kuberi.
5. Kupigana na kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi Mali ya Umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa,Nembo ya Taifa,Fedha ya Taifa,Wimbo wa Taifa na Viongozi wote.
8. Kuoa na kuolewa

9. Kutoa Mimba au kuharibu Mimba ukiwa ndani au nje ya Shule
10. Kupata Mimba au kusababisha Mimba.
11. Kugoma,kuchochea au kuvuruga Amani na Usalama wa Shule na jamii.
12. Kukataa Adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu au kumiliki Simu ya Mkononi, Charger,Line ya Simu na Vifaa vyote vya Umeme.
14. Kulala nje ya Shule bila taarifa/kutoroka.
15. kutokuhudhuria shule kwa siku 90 mfululizo

Mwisho kwa niaba ya jumuiya ya Dareda Sekondari,napenda kukukaribisha sana hapa Shuleni na kukutakia Safari njema na mafanikio mema katika Masomo yako ya Kidato cha V na VI.

Kauli mbiu ya shule yetu ni:

EDUCATION IS THE BEST INVESTMENT na tunakuhitaji uwe na Nidhamu nzuri, juhudi kubwa katika Masomo na tutarajie Matokeo mazuri.

KARIBU SANA DAREDA SEKONDARI.

AHSANTE

.....

SCHOLASTICA L. MUSHI
MKUU WA SHULE.

KIAMBATISHO B.
JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

SHULE YA SEKONDARI DAREDA
S.L.P 344, BABATI-MANYARA
FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE PAMOJA NA MASHARTI YAKE MWAKA 2022.

A: MWANAFUNZI.

Mimi .....nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Dareda.Pia nimesoma na kuelewa vema sheria za shule.Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu zifuatazo:- (Iwapo unakubali nafasi hii toa sababuvivyo hivyo kama unakataa nafasi hii toa sababu).

.....
.....

Tarehe.....Saini.....

B:MZAZI/MLEZI

Mimi.....Mzazi/mlezi wa .....

Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Dareda .Nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema.Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo,ninaahidi/siahidi kumtimizia motto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza,kumlea motto huyu kwa manufaa yake binafsi,wazazi,jamii na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa eleza sababu.

.....

Ahsante.

(i)Jina la mzazi/mlezi wa kiume.....Jina la mzazi/mlezi wa kike.....

Anwani.....

Anwani.....

Namba ya simu ya mkononi.....Namba ya simu ya mkononi.....

Tarehe.....Saini.....Tarehe.....Saini.....

Ndugu/jamaa (3) watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.

N.B Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzi.

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu/jamaa wa karibu ambao wanaoweza kuruhusiwa kumtembelea motto wangu na siyo vinginevyo.

Jina la mzazi/mlezi.....Saini.....

S/N	MAJINA MATATU	UHUSIANO WAKE NA MTOTO	ANWANI	SIMU YA MKONONI	SAHIHI
1.					
2.					
3.					
4.					

***Kata lisilohusika.**

N.B Sehemu 'B'ijazwe na kusainiwa na mzazi na si vinginevyo.

KIAMBATISHO C.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA.

PRESIDENT'S OFFICE.

REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT.

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

DAREDA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 344,
BABATI – MANYARA.
DATE.....

Ref.No.

TO THE MEDICAL OFFICER.

.....

.....

.....(GOVERNMENT HOSPITAL)

STUDEN'S NAME.....AGE.....YEAR.....

Please examine the above named student and arrage for any necessary treatment for student if need be.

.....

Joel .S.Laizer

THE HEAD MASTER.

MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by the medical officer)

I have examined the above named with regard to:

REMARKS.

SKIN.....

EYES.....

EARS.....

TEETH.....

B/S TEST (CHRONIC).....

PRESSURE.....

ABDOMEN.....

CHEST.....

STOMACH.....

URINE.....

H.B HAEMOGLOBIN.....

TB TEST.....

VDRL.....

HIV TEST.....

UPT TEST.....

STOOL.....

ULCERS.....

DIABETIC.....

ASTHMATIC.....

DISABILITIES (If any) .....

ALLERGIES (If any) .....

ADDITIONAL INFORMATION.

Eg.Any physical effects or impartment infections,chronic of family disease etc.

1. The student is in good health free from infection diseases and is fit to proceed with studies.
2. The student will be attendind treatment for.....

SIGNATURE.....

DESIGNATION.....

STATION.....

NOTE: MEDICAL OFFICER.

At the time of Examination, please treat the individual for any ailment you note.

NA.	SOMO	JINA LA KITABU
1.	GEOGRAPHY	i. Practical geography advanced level *Map reading photography interpretation field research, statistics & introductory to survey. ii. Geography an integrated approach –**David Waugh** iii. Physical Geography for Secondary Schools – **D.T-Msabila**
2.	HISTORY	i. Essentials in Advanced level history paper 2, 1&2 **Yassin. S** **ii.** Essentials in advanced level history paper I&II **BY S.YASSIN** iii. Coutemporary historical events paper I&II by tumaini C.K Shibitali iv. Advanced learner's history past I&II by zisti kamili v. Advanced learner's history forms V&VI
3.	GENERAL STUDIES	i. General Studies, Supplementary Book for Advanced Level and Colleges, **-Konrad Adenaker Stiftung, 2nd** Edition
4.	KISWAHILI	i. Nadharia Lugha ya Kiswahili –**Judeck A. Masebo** ii. Uhakiki wa Kiswahili. iii Misingi ya sarufi ya Kiswahili- **mwandishi john** Jitayarishe Kiswahili maswali na majibu nyambari
5.	ENGLISH LANGUAGE	i. Advanced English Language I – **Shadrack Ndambo** ii. Communicative English Language – **Constantine L. Laurence.** iii. English Language II – **Nyambari/Nicholous** iv. Advanced Level Literature Analysis. v. new integrated advanced level English 1 by **Goodluck Mshana**
6	CHEMISTRY	i. Chand 1&2 (Dr J.J Join ii. Ramsden (E.N Ram Sden) iii. Understanding chemistry oxford university
7	Basic And Applied Mathematics (BAM)	i. Basic And Applied Mathematics (BAM) for secondary school K5&K6 TIE ii. Basic And Applied Mathematics (BAM) for Advanced level – Nyambari Nyangwine Publishers –Dar Es Salaam Tanzania
8	BIOLOGY	i. Advanced biology form V student book written by Respicius Rwehumbiza ii. advanced biology form VI student book written by Respicius Rwehumbiza iii. biology principles and processes written by Michael Roberts Michael Rciss GRCE monger